**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 10 – Children to be kept under surveillance if by busy road**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- MFANYAKAZI (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 60-70)

Onyesho la 2:

- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- BWANA WANYAGA (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- DANIEL (MVULANA, UMRI WA MIAKA 6)
- TAYLOR (MVULANA, UMRI WA MIAKA 4)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

Tah: Mtangazaji anaweza kuwa mwanamume na mtaalamu wa usalama barabarani anaweza kuwa mwanamke.

**Intro:**

**1. Beatrice:** Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Jina langu ni Beatrice.Hiki ndicho kipindi chetu cha mwisho miongoni mwa vipindi kumi ambapo tunaandamana na familia ya Wanjiru katika maisha yao ambapo wanashuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Nitazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita Nelson anakataa ushawishi wa rafiki yake, Matthew, na anaamua kununua kofia ya usalama badala ya simu ya kisasa. Saa chache baadaye anaambiwa kwamba Matthew amepata ajali iliyomsababishia majeraha kichwani. Hakuwa amevaa kofia ya usalama.

Katika kipindi hiki Nelson anaitembelea familia ya Nelson inayoishi na iliyo na duka dogo kando ya barabara iliyo na shughuli nyingi mjini.

**<u>Scene One: by the busy road</u>**

**2. SFX Atmo:** **traffic, cars driving past, horns blaring**

**3. NELSON:** Samahani, bwana. Nisamehe kwa kukutatiza kazini. Je unajua nyumbani kwa Wanyaga? Mwanawe anaitwa Matthew.

**4. WORKER:** Eee, naam… Unaona kile kiduka kilicho na kibao cha simu ya mkono. Hiyo ndiyo nyumba yake. Nje unawaona watoto wadogo watatu wakicheza mpira.

**5. NELSON:** Nimeona, asante, … Wale ni wadogo zake Matthew, au?

**6. WORKER:** Naam, ni wadogo zake. Utaniwia radhi acha niendelee na kazi.

**7. NELSON:** Sawa, asante.

**Scene Two: Inside the stall**

**8. SFX Atmo:** **sound of cars passing**

**9. NELSON:** **(Knocking)** Hodi huku! Hamjambo? Jina langu ni Nelson, Matthew ni rafiki yangu. Wewe ndiye Bwana Wanyaga, baba yake Matthew?

**10. MR WANYAGA**: Naam, mimi ndiye babake, na umesema waitwa nani?

**11. NELSON:** Nelson. Tunasoma shule moja na Matthew.

**12. MR WANYAGA:** Aha. Mama ya Matthew amekesha hospitalini pamoja naye. Nami hapa ninashughulikia duka na kuwatunza watoto wetu wadogo. Wanapaswa kuwa skuli lakini kwa kawaida Matthew ndiye anayewapeleka huku mimi na mama yake tukishughulikia biashara.

**13. NELSON:** Tulikuwa na Matthew jana muda mfupi kabla ya ajali. Poleni. Umeshakwenda kumjulia hali hospitalini?

**14. MR WANYAGA:** Naam, jana usiku. Ingawa angali amepoteza fahamu na hata akipata fahamu madaktari wanasema atadumu na ulemavu wa kichwa. Hawajui atakuwa katika hali gani. Nashindwa kujua jinisi hiyo ajali ilivyotokea.

**15. NELSON:** Barabara zenyewe ni hatari na madereva ndio hao tuwajuao wanaoendesha magari kama vichaa. Tena Matthew hakuwa amevaa kofia ya usalama. Natumai atapata nafuu pindi akirejewa na fahamu.

**16. MR WANYAGA:** Ikiwa atapata fahamu… **(worried)** Madaktari wanaonekana kama waliotamaushwa na hali yake. Sijui tufanye nini. Alikuwa akinisaidia kuendesha biashara. Hata hivyo nitaendelea kushughulika ili niwakimu ndugu zake wadogo.

**17. NELSON:** Bila shaka, na wote ni watatu? Wana umri wa miaka mingapi? Si ni hatari kwao kuchezea kando ya barabara bila mwangalizi?

**18. MR WANYAGA:** Inanibidi kuwachunga. Kwa kawaida mama yao anatakiwa kuwepo. Mkubwa wao, Daniel ana umri wa miaka sita na anafahamu mambo kidogo. Lakini hao wengine wawili, Taylor na Thomas, ni mapacha na wana umri wa miaka minne. Nadhani hawana tatizo. Hata hivyo mara nyingine wavulana ni watundu.

**19. NELSON:** Si bora mkajenga ua kuzunguka nyumba yenu ili muwakinge na hatari za barabarani? Haya magari yanaendeshwa kwa kasi sana. Utadhani madereva hawaoni watembeaji kwa miguu au wateja nje ya maduka.

**20. MR WANYAGA:** Ukweli mtupu: madereva wengine wanafikiri kwamba wao ndo wana haki ya kutumia barabara pekee. Mmoja wao ndiye aliyempiga dafrau Matthew. Unajua hata hakusimama? **(sadly)** Alimwacha hapo utadhani mzoga wa mbwa… Siku moja nitaizingira nyumba yangu kwa ua.
Sasa hivi inanibidi kuhakikisha kwamba biashara yangu inaendelea vyema. Wajua pia nanibidi kulipa gharama za hospitali za Matthew.

**21. NELSON:** Bila shaka. Haya, nitakuacha uendelee na kazi. Nimekuja tu kujulia hali ya Matthew. Tafadhali mnijulishe vile anavyoendelea.

**22. MR WANYAGA:** Naam. Kwaheri, Nelson!

**23. NELSON:** Kwaheri Bwana Wanyaga! **(aproaching the kids)** Daniel, nipigie huo mpira!

**24. SFX:** **Sound of football being kicked**

**25. NELSON:** **(shouting)** Simama! Usiukimbilie mpira, gari laja **(Nelson runs)** Simama!

**26. SFX:** **Screech of brakes, Football squashed**

**27. MR WANYAGA:** Kuna nini?

**28. NELSON:** Nimeshika mmoja wa wanao wadogo akiukimbiza mpira barabarani. Hana neno. Ameponea chupuchupu!

**29. DANIEL:** Baba, si mimi, kweli si mimi, sikuliona gari na Taylor ameukimbiza mpira bila kuangalia.

**30. TAYLOR:** Baba, mpira umepasuka. Utatununulia mwingine?

**31. MR WANYAGA:** Haya, acheni. Kila mtu aingie ndani ya duka!

**32. TAYLOR:** Baba, na mpira je?

**33. MR WANYAGA:** Achana na mpira. Matthew angali hospitalini. Hatutaki mkosi mwingine. Niliwaambia nini kuhusu kucheza kando ya barabara?

**34. DANIEL:** Ninajua baba, tujihadhari na magari. Lakini Taylor hakusimama, alikimbia tu kufuata mpira!

**35. MR WANYAGA:** Wewe ndiye mkubwa wao Daniel, unatakikana kuwachunga.

**36. DANIEL:** (Complaining) Lakini baba, siwezi kumkimbiza kila wakati. Unajua kwamba anakimbia upesi.

**37. MR WANYAGA:** **(Sighing)** Najua. Ni kosa langu. Napaswa kuwazuia kucheza kando ya barabara hii yenye shughuli nyingi. Lau Matthew na mama yenu wangekuwa hapa ingekuwa rahisi zaidi kuwachunga. Nelson unayosema ni kweli. Ninapaswa kuizingira nyumba yangu kwa ua.

**END OF SCENE TWO**

**SHORT MUSIC**

**38. BEATRICE:** Kama mlivyosikia katika kipindi hiki cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama, kufiki sasa, wazazi wake Matthew hawajachukulia kwa uzito usalama wa watoto wao wanaocheza kando kando ya barabara. Hapa studioni ninajiunga naye George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. George karibu!

**39. GEORGE:** Asante.

**40. BEATRICE:** Bila shaka, George, ndugu zake Matthew wameponea chupuchupu na nafuu kwa baba yake Matthew. Mwanawe mmoja yuko hosiptalini na mwengine nusura apate ajali.

**41. GEORGE:** Ndiyo. Mtazamo wa Nelson kuhusu matumizi ya barabara umebadilisha mkondo wa mambo katika mchezo huu wa redio. Anafahamu sana suala la usalama barabarani. Hata alipokwenda nyumbani kwa kina Matthew na kuwaona ndugu zake wadogo wakicheza kando ya barabara hakukosa kumtahadharisha baba yao.

**42. BEATRICE:** Alielewa vizuri hatma ya watoto hao barabarani.

**43. GEORGE:** Ndiyo alielewa, ndiposa akampendekezea babake Matthew kuizingira nyumbani yake kwa ua. Lakini kama tulivoyjifunza kwenye mchezo huu wa redio majuto huja kinyume. Watu wanapopata ajali ndipo wanapotanabahi kuhusu sababu za ajali hizo. Mfano mzuri ni huyo babake Matthew. Taylor anapokaribia kupigwa dafrau anapokimbiza mpira barabarani ndipo babake Matthew anapotambuwa hatari inayowakabili wanawe na pia anakumbuka suala la usalama barabarani.

**44. BEATRICE:** Tena ni kosa kubwa kuwaachia watoto wadogo wacheze kando ya barabara bila kuzingatia kwamba huenda wangeukimbiza mpira barabarani.

**45. GEORGE:** Watoto wadogo hawajui hatari zinazowakabili. Hawaoni kama mikasa inaweza kuwasibu. Ni jukumu la wazazi kuwachunga. Hatuna budi kuwatunza watoto wetu na hasa kama tunaishi kando ya barabara yenye shughuli nyingi, wazazi wanapaswa kuhakikisha kwamba watoto wana eneo salama la kuchezea. Na iwapo hatuwezi kuwachunga vilivyo, bora tuweke ua, ama wacheze upande wa nyuma wa nyumba. Wazazi wanapaswa kujitahidi vyovyote kuhakikisha usalama wa watoto wao kutoka na hatari za magari barabarani.

**46. BEATRICE:** Asante George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)<u>OUTRO</u>**

**47. BEATRICE:** Hicho kilikuwa kipindi cha mwisho cha mfululuzo wa vipindi kuhusu usalama barabarani. Tunatumaini kwamba umejifunza na umefurahia michezo yetu ya redio iliyoandikwa na Victoria Averill.

Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au vipindi vingine vya mfululizo huu wa vipindi, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe.

Je tumefanikiwa kuzifanya shughuli zako barabarani salama zaidi? Tuletee maoni yako kuhusu hiki kipindi

Tuandikie barua pepe kwa kutumia anwani ifuatayo lbe@dw.de

Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabani!